# Hadithi 31

## MIONGONI MWA AINA ZA MAKADIRIO YALIYOTANGULIA

Kutoka kwa Abdullah bun Masood, amesema: alitwambia Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) – na yeye ndiye mkweli anae kubalika -

1. Hakika mmoja wenu hukaa katika tumbo la mama yake siku arobaini, kisha anakuwa pande la damu kwa siku nyingine kama hizo, kisha anakuwa pande la nyama kwa siku nyingine kama hizo

2. Kisha Mwenyezi Mungu anamtuma malaika kwa ajili ya mambo manne, aandike matendo yake, kifo chake, riziki yake na atakuwa mwema au muovu

3. Kisha anapuliziwa roho.

4. Kwa hakika mtu anaweza kufanya matendo ya watu wa Motoni mpaka inabaki baina yake na kuingia Motoni kiasi cha dhiraa urefu wa mkono kutoka kwenye kiganja mpaka kwenye kiwiko, mipango ya Mwenyezi Mungu inamtangulia, anatenda matendo ya watu wa Peponi, anaingia Peponi.

5. Na hakika mtu anaweza kufanya matendo ya watu wa Peponi mpaka inabaki baina yake na kuingia Peponi kiasi cha dhiraa, mipango ya mwenyezi mungu inamtangulia, anatenda matendo ya watu wa Motoni, anaingia Motoni" imepokelewa na Bukhari Na Muslimu.[1]

1 Al-Bukhari (3332) na Muslim (2643).

### Ayah

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu

*﴿Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo. 13. Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti. 14. Kisha tukaiumba tone kuwa damu iliyoganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe mwengine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji. 15. Kisha hakika nyinyi baada ya hayo mtakufa. 16. Kisha hakika nyinyi Siku ya Kiyama mtafufuliwa﴾ [muuminuun: 12-16].*

*﴿Ambaye ametengeneza vizuri umbo la kila kitu; na akaanzisha kumuumba mtu kwa udongo. 8. Na kisha akajaalia uzao wake utokane na kizazi cha maji madhaifu. 9. Kisha akamtengeneza, na akampulizia roho yake, na akakujaalieni kusikia na kuona, na nyoyo za kufahamu. Ni uchache mnavyo shukuru﴾ [Al-Sajdah: 7-9]*

*﴿Na wanakuuliza khabari za Roho. Sema: Roho ni katika mambo ya Mola wangu Mlezi. Nanyi hamkupewa katika ilimu ila kidogo tu﴾ [Al-Isra: 85].*

*﴿Na katika watu wapo wanao muabudu Mwenyezi Mungu kwa ukingoni. Ikimfikia kheri hutulia kwayo, na ukimfikia msukosuko hugeuza uso wake. Amekhasiri dunia na Akhera; hiyo ndiyo khasara iliyo wazi. [Hajj: 11].*

*﴿Na jengo lao hilo walilo lijenga litakuwa sababu ya kutia wasiwasi nyoyoni mwao mpaka nyoyo zao hizo zikatike vipande vipande. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima﴾ [At-Tawbah: 115].*

### Msimulizi

Ni baba Abdur Rahmaan, Abdullah bun Masood bun Ghaafil bun Habibu, ukoo wa Hudhali, ni swahaba wa Mtume Mtukufu, alisilimu mapema Makka, na ni wakwanza aliye isoma Qur`ani wazi kwa sauti Makka, alihama mara mbili (Ethiopia na Makka), alishiriki vita ya Badri na nyingine zote pamoja na mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake), na alikuwa ndiye msimamizi wa viatu vya Mtume Mtukufu, anampatia anapotaka kutoka, na kuvibeba anapo rudi, alifariki katika mji wa Madina mwaka (32H) au (33H) [1].

### Muhtasari

Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) ametaja katika hadithi hii baadhi ya hatua za ukuwaji wa kijusi katika tumbo la mama, kupuliziwa roho na kuandikiwa mambo yake yote.

Kisha akabainisha kwamba kinacho zingatiwa katika matendo yake ni mwisho, mwenye kuhitimisha uhai wake kwa matendo ya watu wa Peponi, basi atakuwa miongoni mwao, na mwenye kuhitimisha uhai wake kwa matendo ya watu wa Motoni, basi atakuwa miongoni mwao.

1 Rejea yake ufafanuzi wake katika: "Maarifaat al-Sahaba" na Abu Nu'aym (4/1846), "aliastieab fi maerifat al'ashabi"na Ibn Abd al-Bar (4/1770), "Asad al-Ghaba" na Ibn al-Atheer (3/357), "Al-Isbah fi Tamazu al-Sahaba" cha Ibn Hajari Asqalani (4/267) .

# Ufahamu

1 Abdullah bin Masood anatuelezea hadithi ambayo baadhi ya vipengele vyake ni mambo ya siri ambayo hakuna anaye jua uhalisia wake ila Mwenyezi Mungu Mtukufu, ndio maana akasema: (na yeye ndiye mkweli anaekubalika) sawa sawa katika mambo ya wazi au siri.

Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) anaelezea hali za kijusi na hatua za kuumbika kwake katika tumbo la mama. Anakuwa ni tone la maji, maji ya uzazi ya baba na yai la mama, na eneo la kuumbiwa ni katika kizazi cha mama, kisha anakuwa pande la damu lililoganda, linaitwa a'laqah, yaani kinachoganda au kuning'inia, na limeitwa hivyo kwa sababu huwa linaganda katika kuta za kizazi, kisha linakuwa pande la nyama, ni kipande cha nyama kidogo kiasi ambacho inawezekana kukitafuna mdomoni.

2 Baada ya kuwa pande la nyama, Mwenyezi mungu anamuamrisha malaika msimamizi wa vizazi, yaani viumbe pindi wanapokuwa tumboni kwa mama, aandike mambo yake yote, anaandika riziki yake, kifo chake, matendo yake na atakuwa mwema au muovu.

Lakini pia huwa anaandika mambo zaidi ya hayo, kama vile, atakuwa jinsia ya kike au kiume,[1] tabia zake na maumbile yake[2]. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) aliyataja hayo mambo manne kwa sababu mengine yanaingia ndani yake , na kwa kuzingatia umuhimu wake. Haya anayoyaandika malaika si aliyoyaandika Mwenyezi Mungu katika Lauhul mahfuudh (palipo andikwa mambo yote yanayotokea), haya anayoyaandika malaika, kuna uwezekano wa kufutwa au kurekebishwa au kubadilishwa kwa sababu alizoziweka Mwenyezi Mungu, kama dua na matendo mema, tofauti na aliyoyathibitisha Mwenyezi Mungu katika Lauhul mahfuudh, hayo haiwezekani kuyabadilisha wala kuyarekebisha. Amesema Mwenyezi Mungu: ". Mwenyezi Mungu hufuta na huthibitisha ayatakayo. Na asili ya hukumu zote iko kwake. [Al-Ra'd: 39] [3].

3 Hapo ndipo Mwenyezi Mungu anapulizia kijusi roho na kinakuwa hai kwa uwezo wake Mtukufu. Kupulizia roho ni katika mambo ya ghaibu ambayo anayajua Mwenyezi Mungu pekee, na amelificha viumbe wake wasilijue, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: " Na wanakuuliza khabari za Roho. Sema: Roho ni katika mambo ya Mola wangu Mlezi. Nanyi hamkupewa katika ilimu ila kidogo tu. [Al-Isra: 85 , Bali sisi wajibu wetu ni kuamini kwa yakini alichokielezea Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) kutoka kwa Mola wake kwamba " Hakika amri yake anapotaka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa. " [yasin: 82].


1 Al-Bukhari (3333) na Muslim (2646).

2 Ishaq bin Rahwayh katika "Musnad" yake (2/344), na al-Ajri katika "Shari'ah" (365). Al-Haythami aliisahihisha katika "Majma' Al-Zawa'id na Manbi Al-Fawa'id" (7/193).

3 Tazama: "sherh ya arobaini al-Nawawi" cha Ibn Rajab (uk. 45), "Fath al-Bari" cha Ibn Hajar (11/485).

Hayo yote hutokea pindi pande la nyama linapo kuwa kikamilifu na kutengeneza umbile la binadamu, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: “5. Enyi watu! Ikiwa nyinyi mna shaka ya kufufuliwa basi kwa hakika Sisi tulikuumbeni kutokana na udongo, kisha kutokana na manii, kisha kutokana na kipande cha damu ilio gandana, kisha kutokana na kipande cha nyama chenye umbo na kisicho kuwa na umbo”, [Hajj: 5] Pande la nyama lililo jiweka katika Umbile, ni lililo umbika kikamilifu, katika sura ya binadamu, na pande la nyama ambalo halijajiweka katika umbile, ni ambalo alijaumbika kikamilifu katika sura ya binadamu, hili huwa linaporomoka, inakuwa ni mimba iliyotoka[1].

4 Kisha Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akaeleza kwamba, kinachozingatiwa katika matendo ni mwisho wake, na yote yaliyotangulia yanabaki katika elimu ya Mwenyezi Mungu na jinsi alivyoandika ubaya au uzuri kwa mja. Huenda mtu akatenda matendo ya watu wa Motoni kwa muda Mrefu mpaka kifo chake kinapokaribia, Mwenyezi Mungu anamuafikisha, anatubia na anamsamehe na kuhitimisha uhai wake kwa matendo mema na kuingia Peponi, kwa sababu Mwenyezi Mungu alishaandika katika Lauhul mahfuudh (palipoandikwa mambo yote yanayotokea), na katika tumbo la mama yake alipo muagiza malaika, kwamba atakuwa mwema.



1 Tazama: “Al-Mufhim lamaa ‘ashakil min talkhis kitab muslimin” cha Al-Qurtubi (6/651).

5 Na kinyume chake, mtu anaweza kutenda matendo ya watu wa Peponi kwa muda mrefu, mpaka anakaribia kuingia Peponi kwa kukaribia kifo chake, lakini anatanguliwa na aliyo yaandika Mwenyezi Mungu kwamba atakuwa muovu, anatenda matendo ya watu wa Motoni na anakufa katika hali hiyo na kuwa katika watu wa Motoni. Hii haimanishi kwamba muumini anaweza kupotea baada ya kuongoka bila sababu kutoka kwake mwenyewe. Hayo yote ni kwa hekima na uadilifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa mfano, mtu anaye muabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu bila elimu, kwa jinsi anavyo jisikia, akipatwa na kheri anashukuru, ikiwa kinyume anakufuru, kama alivyo sema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na katika watu wapo wanaomuabudu Mwenyezi Mungu kwa ukingoni. Ikimfikia kheri hutulia kwayo, na ukimfikia msukosuko hugeuza uso wake. Amekhasiri dunia na Akhera; hiyo ndiyo khasara iliyo wazi. [Hajj: 11]

Na mfano ni mnafiki, katika hadithi: "Mtu anaweza kutenda matendo ya watu wa Peponi – katika macho ya watu – hali ya kuwa ni mtu wa Motoni, na mtu anaweza kutenda matendo ya watu wa Motoni – katika macho ya watu – hali ya kuwa ni mtu wa Peponi"[1]. Na mwisho wa uhai kama huu, kwa mtu ambaye kwa muonekano ni mwema, ni katika matukio adimu sana yasiyo onekana mara kwa mara, na hekima yake ni kuonesha kwamba, katika matendo kinachozingatiwa ni mwisho wake, na mwanadamu kamwe asijidangaye kwa wingi wa ibada na matendo yake mazuri. Hii ni miongoni mwa huruma za Mwenyezi Mungu, kwani watu kutubia na kuacha maovu inatokea kwa wingi sana, ama kubadilika na kuwa waovu ni nadra, ingelikuwa ni kinyume, watu wangelipata Mtihani mkubwa sana[2].

Mara nyingi inavyojulikana ni kwamba watu wema huwafikishwa kutenda mema, na waovu hutenda maovu, kama ilivyobainishwa katika hadithi kwamba Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) anasema: "hakuna yeyote kati yenu wala yeyote ambeye amepuliziwa uhai, ila huandikwa nafasi yake Peponi na nafasi yake Motoni, japo imeandikwa kuwa ni mwema au muovu", bwana mmoja akasema: eh Mtume wa Mwenyezi Mungu, si tuache kutenda mema na tusubiri matokeo kama ilivyoandikwa? Atakae kuwa ni mwema, ataingia katika wema, na atakae kuwa ni muovu, ataingia katika waovu, Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akasema: "wema watawekewa wepesi kufanya mema, na waovu watawekewa wepesi kufanya maovu" kisha akasoma: "Na akaliwafiki lilio jema, " [Alliyl: 6][3]

1 Al-Bukhari (2898) na Muslim (112) kutoka katika Hadithi ya Sahel bin Saad Al-Saadi, M/Mungu amuwiye radhi.
2 Ufafanuzi wa Arobaini Al-Nawawi cha Ibn Daqiq Al-Eid (uk. 39).
3 Al-Bukhari (1362) na Muslim (2647).



# Mafunzo

1. Amesema Ibn masood, katika kuelezea sifa ya Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake): “mkweli anaekubalika”, hii ni kuonesha jinsi alivyomuamini, kumkubali na kutekeleza aliyo kuja nayo kikamilifu hata kama akielezea mambo ambayo yako kinyume kiakili, au juu ya uwezo wa akili kuyakubali au kuyakanusha katika mambo ya ghaibu. Na ndio maana maswahaba ni watu bora baada ya manabii, na kiigizo cha waumini katika kumuamni Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) na kufuata mafundisho yake.

2. Ameeleza Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) hatua za ukuaji wa kijusi katika tumbo la mama kabla ya teknolojia ya kitabibu na vifaa vya kisasa vilivyothibitisha ukweli wa maneno ya Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake). Jambo hili ni katika mambo yenye kumzidishia muumini Imani, pindi anapoona Sayansi inathibitisha kilichoelezewa katika Qur`ani na mafundisho ya Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) na wala hakuna mgongano wowote.

3. Tizama uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kubadilisha kijusi katika hatua tofauti tofauti, na katika kupanga mipango kwa njia nzuri yenye kustaajabisha. Mfano wa mambo kama haya yanapelekea kumtukuza Mwenyezi Mungu zaidi na kujisalimisha kwake.

4. Lau mwanadamu angezingatia na kujua hekima ya kuumbwa mwanadamu hatua kwa hatua, na hali ya kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ana uwezo wa kukiambia kitu: kuwa na kikawa jinsi atakavyo. Hii ni kuilea nafsi iwe na utulivu na umakini, na isiwe na papara katika mambo na kutaka matokeo ya haraka, kama inavyotuonesha mahusiano makubwa aliyo yaweka Mwenyezi Mungu (Rehma na Amani ziwe juu yake) baina ya kufanya sababu na kupata matokeo yake kwa kuzingatia utaratibu wa kilimwengu.

5. Ukipatwa na jambo katika kazi yako, au riziki yako, au ukatamani upate jambo ambalo hauna, usihangaike kulaumu Qadar yaani mipango ya Mwenyezi Mungu, au kujuta na kuishusha nafsi, bali ridhia alichokuandikia Mwenyezi Mungu Mtukufu, na utambue kwamba ameliandika ukiwa katika tumbo la mama, na kabla ya kuingia katika tumbo la mama Hakuna zaidi ya kujisalimisha kwake na kufanya anayoyaridhia.

6. Haifai kwa mwanadamu kumuhukumu yeyote kuwa ni mtu wa Peponi au Motoni, kwa sababu hilo ni la Mwenyezi Mungu pekee, na yeye ndiye ameandika matendo yote ya waja, muovu anaweza akawa mwema, na mwema anaweza akawa muovu.


7. Haifai kwa mwanadamu kubweteka na matendo yake na kuacha jitihada, kwa sababu kinachozingatiwa katika matendo ni mwisho wake. Sufian Athauriy - Mwenyezi Mungu amrehemu – alikuwa analia akisema: “naogopea isije ikawa katika lauhul mahafudh yaani

palipoandikwa mambo yote yanayotokea, imeandikwa kwamba mimi ni muovu", na alikuwa akisema: "naogopea kupokonywa Imani kabla ya kifo changu"[1].

8 Inatakiwa kwa mwislaam adumu katika kumuomba Mwenyezi Mungu amdumishe katika kumtii, na wala asimpoteze na akateleza. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alikuwa akikithirisha kusema: "Eh mwenye kubadisha nyoyo, nakuomba uudumishe moyo wangu katika dini yako"[2]

9 Ameeleza Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) kwamba, kuna mtu alisema: "ninaapa, Mwenyezi Mungu hatamsamehe fulani" na Mwenyezi Mungu akasema: "ni nani anaapa juu yangu kwamba sitamsamehe fulani?! Kwa hakika nimesamehe na nimekufutia mema yako"[3].

10 Amesema Ally bin Abuu Twaalib: "jiepusheni kuwaiga watu, kwa sababu, mtu anaweza kutenda matendo ya watu wa Peponi kisha anabadilika, - kwa jinsi Mwenyezi Mungu anavyo juwa uhalisia wake – anatenda matendo ya watu wa Motoni, ana kufa akiwa katika watu wa Motoni, na mtu anaweza kutenda matendo ya watu wa Motoni kisha anabadilika - kwa jinsi Mwenyezi Mungu anavyo juwa uhalisia wake – anatenda matendo ya watu wa Peponi, anakufa na akiwa katika watu wa Peponi. Ikiwa hamna budi zaidi ya kumuiga, basi muige ambao walio kwisha tangulia mbele ya haki na wala si walio hai[4].



**Amesema mshairi:**

*Katika ulimwengu Mwenyezi Mungu ana dalili zinazo thibitsha uwepo wake***huenda ndogo kabisa ndiyo aliyo ifanyaiwe sababu ya wewe kuongoka.*

*Huenda dalili za uwepo wake zilizopo katika nafsi***ni maajabu makubwa lau jicho lako likizama kwa mazingatio.*

*Na ulimwengu umejaa siri***kama jicho lako likitizama kwa kutaka undani wake.*

*Kiulize kijusi kinacho ishi peke yake***bila msimamizi wala chakula, ni nani ana kusimamia?*

1 Ufafanuzi wa Arobaini Al-Nawawi cha Ibn Rajab (uk. 47).

2 Al-Tirmidhiy (2140), Ibn Majah (3834), kwa kutoka kwa Anas bin Malik, Al-Tirmidhiy amesema: Ni Hadithi nzuri.

3 Muslim (2621), kutoka kwa Jundub bin Abdullah

4 "i`ilam almuqiiin an rabi a`la amina"" na Ibn al-Qayyim (2/135).

